

## **Sarafu ya Dhahabu Ambayo haikutoa mlio wa kweli**

Abdullah aliishi katika nyumba yake pembezoni mwa kijiji. Alipata mapato yake kwa kuuza mboga sokoni, ambazo alikua katika ardhi yake ndogo. Alifanya kazi hii tangu alipokuwa yatima kama mtoto mdogo.

Jinsi siku zilivyokuwa zikienda, umri nao uliendelea. Sasa hakuweza tena kulima, kupanda, kupalilia, na kumwagilia vimekuwa kazi kubwa sana kwake. Hakuwa na wasiwasi tu kwa ajili ya kipato kwa maisha yake lakini pia jinsi atakavyolipa kodi.

Kila yalipofika majira ya wakati wa kulipa kodi alipewa taarifa ya kulipa. Kwa kawaida aliiweka taarifa hiyo pemberi mpaka alipopata fedha toka mauzo ya mazao kulipa kiasi kilichohitajiwa. Lakini mwaka huu ilikuwa tofauti. Kulikuwa na ukame. Mazao mingi yalipukutika na mavuno yake hayakuweza hata kujaza kikapu kimoja.

Siku moja, mtoza kodi alifika na kumpa taarifa ya pili. Kwa kawaida, Abdullah alijawa na mashaka juu ya kulipa kodi. Alifikiria kukopa fehda kwa majirani lakini akaona kwamba hata hao hali ilikuwa ngumu pia. Hakuwa na njia nyingine yoyote ya kufanya.

Hali ikaendelea kuwa mabaya zaidi. Kuta za nyumba yake zilichakaa na zilihitaji ukarabati. Alipokuwa akipiga lipu, aligundua chungu kilichokuwa kimefichwa ndani katika sehemu ya ukuta mmoja. Kwa furaha, aliitoa na kumwaga chini vile vilivyomo ili aone kuna nini. Makaratasi yakatawanyika alipokuwa akiyashika lakini mwisho chini ya chungu akaona sarafu ya zamani sana. Alipochunguza na kuifuta, ikang'aa kama dhahabu. Mawazo lake la kwanza lilikuwa, "Sasa nitaweza kulipa kodi!" Akatulia. Alikuwa na matazamio makubwa ya kulipa na fedha nyingine kubaki, aliwasha sigara yake na kuivuta kwa utulivu mkubwa.

Jioni ileile mtoza kodi, ambaye pia alikuwa rafiki yake alimpitia na kumsalimia akitaka pia kujua mambo yake yanaendeleaaje. Alijua kabisa kwamba kwa kuzingatia kazi yake angetazamia kumletea Abdullah taarifa ya mwisho ili aliye kodi. Baada ya mazungumzo ya kirafiki, Abdullah alimwambia yule mtoza kodi juu ya sarafu ya "dhahabu". Yule mtoza kodi alimwomba ili aiangalie. Ile sarafu ilipoletwa, mtoza kodi akairusha kwenye jiwe ili askie kama itatoa mlio wa kweli. Akamrudia Abdullah na sura ya simanzi, na kusema, "Sarafu hii haitoi mlio wa kweli, rafiki yangu."

"Kwani hii haikuja kutoka kwa mababu na hata pengine na wao toka kwa mababu zao miaka mingi iliopita? Unawezaje kusema leo kwamba sarafu hii si nzuri?", aliuliza Abdullah.

Yule mtoza kodi akaigeuzageuza ile sarafu na kuiangalia tena na tena, akamwabia, "Kwa sehemu ni nzuri, lakini kwa sehemu ni mbaya. Haitachukuliwa utakapoitoa."

Abdullah alikasirika sana na kusema, "Unawezaje kuwadharau mababu zangu na kuharibu majina yao mazuri! Unadhani wao hawakujua kati ya sarafu nzuri na mbaya?"

Mtoza kodi akamjibu kwa utulivu na kwa upole, "Mimi sijui lolote kuhusu mababu zako mpendwa kaka yangu, lakini najua kwa hakika kwamba sarafu hii haiotoi mlio wa kweli na kwamba haitachukuliwa utakapoitoa. Kama sitakuonya na eunde mahakamani, mimi sitakuwa rafiki mzuri."

Kuskia hivyo, Abdullah akasirika zaidi na hata kukataa kuzungumza na rafiki yake. Mtoza kodi aliamka, akamwaga na kuondoka.

Usiku ule Abdullah hakulala kwa sababu alijawa na wasiwasi na mashaka. Akasema peke yake, "Hivi Baba yangu na baba zake wangetunza sarafu ambayo haikuwa halisi?" Alimaliza kwamba wasingeweza kutunza sarafu isiyio na thamani. Baada ya kujiliwaza na mawazo haya, amani ikarudi moyoni mwake na akaamua kutofikiria jambo hilo tena.

Katika hali hii, hakufanya juhudini zozote za kujuwa ukweli wa ile sarafu mpaka siku ya malipo. Wala hakufikiria kwamba nini kinaweza kutokea kama haitakuwa na thamani na kushindwa kulipa kodi. Hatimaye, taarifa ya mwisho ya kulipa kodi ikaja.

Akaichukua sarafu ya "dhahabu" inayong'ara, Abdullah akaenda katika ofisi ya kulipa na kujipanga mstari ili akalipe. Kama mtoza kodi alivyomwambia, mpokea fedha akaichukua ile sarafu akaitupa chini katika jiwe aone kama itatoa mlion wa kweli. Ilitoa mlion mzito sana. Mpokea fedha akamrudishia Abdullah sarafu yake na kumwambia, "Kaka yangu sarafu hii haitoi mlion wa kweli; tafadhali toa nyingine".

Sura ya Abdullah ikabadilika. Akajibu "Sina nyingine. Ninakuomba, Bwana wangu chukua hii kwa dhamani yoyote ile; ingawa ni chuma imechanganywa lakini kipande kikubwa kama hiki lazima kiwe na thamani yake".

Mpokea fedha akamjibu, "Hakuna shaka kwamba ndani yake kuna dhahabu kidogo, lakini yote imechanganywa na vitu visivyo na thamani. Siwezi nikakubali". Unajua kwamba serikali inataka malipo kwa dhahabu safi. Nakupa siku tatu kuja na malipo halisi. Hicho ndicho utakachofanya".

Abdullah hakuwa na maneno la kusema. Kwa kiburi chake hakuweza tena kwenda kwa mtoza kodi kukiri kuwa alikuwa mpumbavu kuthamii sarafu ambayo haikuwa na thamani. Aliona nikujishusha kuomba msaada. Katika kipindi cha zile siku tatu hakuna alichoweza kufanya. Siku ya nne, polisi walikuwa wakampeleka gerezani. Alipokuwa akipelekwa gerezani majirani zake walimsikia akisema, "Ulikuwa ujinga wangu mwenyewe. Adhabu yangu ni juu ya kichwa changu. Nilithamini sarafu ambayo haikutoa mlion wa kweli".

*Rafiki, je unashangazwa na Abdullah ambaye hakuwa mwaminifu? Ni afadhali tuangalie deni tunalodaiwa na Mungu, Bwana wa ulimwengu wote, na kuchunguza maonyoambayo ametupa. Mungu wa mbinguni anampa kila mmoja wetu maonyo matatu kwamba ni lazima tufike mbele zake siku ya hukumu. Onyo la kwanza ni juu ya sauti nafsini mwetu. Mungu anatuonya kwa njia ya nafsi zetu kwamba tukifanya makosa atatuadhibu. Hii ni kama ile taarifa ya kwanza kwa Abdullah. Onyo la pili linaoka katika Neno la Mungu lililoandikwa linalofundishwa waziwazi kwamba kifo ni tokeo la dhambi, na baada ya kifo kunakua hukumu. Onyo la tatu ni gumu zaidi. Ugonjwa unapokuja, kifo kinaonekana kuwa karibu, inakuwa wazi zaidi kwamba tunaenda kukutana na kujibu kwa kila kitu tulichofanya. Kwa maneno mengine, tutalazimika kwenda kulipa, kama Abdullah.*

*Ni wakati wa kujichunguza mwenyewe katika mai-sha yako. Katika kile unachoamini. Je, kitatoa mlion wa kweli mbele za Mungu siku ya hukumu?*

*Unaweza kuamini katika namna ulivyokadhibiwa na mababa zako, ukidhani kuwa ni kitu cha kweli. Mpendwa rafiki yangu, pima dini yako, uone kama ni halisi; kama kweli itakupitisha Siku ya Hukumu ya Mungu. Mungu anataka kwamba kila sala isemwe kwa moyo ulio safi, huru toka mambo ya kujipendez nafsi au hasira au chuki. Sala yako imekuwa "dhahabu safi?"*

*Haijalishi tunajaribu kiasi gani, au tunasema sala zetu mara ngapi, kutoa kwa masikini, kufunga, kwenda kuhiji, tunarudi katika tatizo lilelile. Katika Biblia Takatifu tunasoma: "Hakuna mwenye*

*haki, hata mmoja; hakuna afahamuye Mungu. Wote wamepotoka, wameoza wote pia; hakuna mtenda mema, la! Hata mmoja". (Warumi 3: 10-12)*

*Vitabu vitakatifu na mioyo yetu, tunapokuwa wakweli, vinatuambia kwamba tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Hivyo, kuamini juu ya dhana ya sarafu nzuri ni kuamini sarafu isiyokuwa ya kweli. Lakini Mungu hajatuacha katika hali hii mbaya. Ni maisha yang'arayo, dhahabu halisi ya maisha isiyo na dhambi-maisha ya Yesu, Masihi. Alijitoa ma-hali pako kama malipo halisi (dhabihu) kwa ajili ya dhambi yako. Maisha yake matakatifu yanamridhisha Mungu kwa ajili ya dhabihu safi ili kufikia hitaji la sheria halisi. Ufufuo wake toka katika wafu ulikuwa mkamilifu na usiokatalika kwa ajili ya uthibitisho huu.*

*Ukimwamini Yesu Masihi kwa moyo wako wote, kitu cha ajabu kitatokea. Kile ambacho us-ingeweza kufanya wewe mwenyewe yeye atakufanyia. Wewe ni mnyonge; yeye ni mwenye nguvu. Unafanya dhambi; Yeye hana dhambi. Alikufa badala yako kukuokoa toka adhabu ya milele.*

*Unapomwamini kwa hakika kama Mwokozi na Bwana, Anasafisha dhambi zako za kale na kumtu-ma Roho wake Mtakatifu kuishi ndani yako. Anakupa asili mpya, na kukusaidia kujifunza maisha mapya kwa ajili ya Mungu. Badala ya kuleta matendo yako mbele ya Mungu (sarafu isiyo na thamani), yeye anakupa nguvu mpya uishi kama mtoto wa Mungu, na kuingia kwa maisha ya milele Mbinguni. Kwa hiyo, rafiki yangu, tupa sarafu isiyo na dhamani ambayo pengine unaiamini. Na badala yake, pokea kwa imani dhahabu safi, Masihi asiye na dhambi, kama Bwana na Mwokozi wako.*

---

**“Sarafu hii haitoi mlion wa kweli, rafiki yangu”**

Kukusaidia kuelewa zaidi kuhusu Yesu Masihi,  
tuko tayari kukutumia vijitabu vingine.  
Tafadhali wasiliana nasi kupitia anuani zifuatazo:

### **HAMASA YA MILELE**

Box 11795 Arusha, Tanzania

Simu: **0767-288053, 0784-288053**

Barua pepe: [hymilele@gmail.com](mailto:hymilele@gmail.com)

### **LIFE CHALLENGE**

Box 50770, Nairobi, Kenya

Simu: **0728-858.333**

Barua pepe: [coast@lifechallenge.de](mailto:coast@lifechallenge.de)